

NILIMDHANIA KAHABA KUMBE BIKRA

MTUNZI: SINGANOJR .

Mono no aware

ILIPOISHIA

Upande mwingine katika ulimwengu
unaojitegemea watu wote walijikuta wakisimama
wasiamini macho yao .

Hata kwa Sharif na Aoiline wote walisimama kwa
pupa wakimwangalia Roma akikiendea kifo kwa
mshangao mkubwa na kutokuamini.

“What the hell is he thinking ...”Sharif hakujua akasirike , achanganyikiwe au ni hisia gani nyingine ambazo zilimsababishia kukunja ngumi yake kama mwanamasumbwi anaetaka kuingia ulingoni., hisia zake alishindwa kuzitawala jambo ambalo ni nadra sana kwake.

Aoiline bila kutarajia na pengine kwa zaidi ya miaka mingi sana hakuwahi kutoa machozi lakini muda huo machozi yaliufunuka uso wake mzuri sana na kumzidi kupendeza na kusikitisha kwa wakati mmoja.

“Amefikiria nini huyu mtukutu... kwanini kafanya maamuzi ya kijinga namna hio?”Ndio kauli pekee alioweza kuongea huku akipaliwa na mate.

Upande wa Clark alikuwa ashajipigia magoti huku akitoa kilio cha kwikwi , uso wake wa kirembo ulifubaa kama vile umekosa virutubisho kwa muda mrefu , aliishia kufumba macho yake akiwa na majonzi makuu huku aking’ata lipsi

zake kiasi cha kujitoa damu , alitingisha kichwa chake kwa majonzi makubwa ya kutokukubali.

“I Knew it .. I knew it ..” Aliongea akimaanisha alijua , alijua juu ya hilo lakini ilikuwa ameshachelewa kuongea neno hilo.

Maamuzi ya Roma yalikuwa ni nje ya matarajio ya kila mmoja .

“Wh.. Why..?!”

“Kwanini?”

Katika ubaridi huo wa upepo Athena alijikuta kwa kutetemeka midomo kama mgonjwa wa malaria alimuuliza Roma kwanini kafanya hivyo , macho yake yalikuwa makavu kama kioo akiwa bado ni mwenye kushindwa kuamini uhalisia uliokuwa mbele ya macho yake.

SEHEMU YA 796.

Athena alijihisi ni kama nguvu zake zote zinampotea kutoka katika mwili wake, ukiachana

na kuongea kauli hio ya kuuliza akili yake
haikuwa ikifanya kazi kisawasawa.

Wakati wa unabii wake kushindwa kutabiri kwa
usahihi , hatimae pigo kubwa linampata , akili
yake ilirudi katika uhalisia na kujua nini
kimetokea.

Kwa sababu ambazo hazikujulikana alikwepesha
macho yake na ya Roma na hakuweza hata
kuangalia jeraha ambalo amemsababishia ,lakini
vilevile hakuelewa kwanini katika wakati huo
alikuwa akitaka kulia.

Mara baada ya tone la chozi kumdondoka na
kuyafikia mashavu yake , kwa upole lilifutwa na
vidole vya Roma.

“Nini tatizo ?, unalia..?” Aliuliza Roma akiwa ni
mwenye tabasamu hafifu.

Licha ya damu nyingi kutoka katika eneo la
moyo , bado alikuwa katika hali ya utulivu na
hakuonyesha ishara yoyote ya maumivu , ni kope

za macho tu ambazo ndio zilikuwa zikicheza
cheza kwa haraka.

“Unaniuliza kwanini nimefanya hivi? , kwani
sijakuambia kwamba ni jambo ambalo
limekwisha kupangwa , kwasababu hutaki
kuacha na siwezi kukuua vilevile basi mimi ndio
nakufa , kama nikifa sitowajibika tena ,
sitomuangusha yoyote na ukweli sitokuwa na
haja ya kujali sana haya mambo , pia
sitojihangaisha na mambo yako ambayo unafanya
.. kwa maana kwamba utaweza kuishi vizuri
mimi nikiwa mfu”

Athena alijaribu kukizungusha kichwa chake
pembeni akijitahidi machozi yasimtoke lakini
alikuwa akishindwa.

Mkono wake ambao ulikuwa umeshikilia mkuki
hatimae ulikosa nguvu zote na kuanza
kutetemeka na alijkuta akiachia .

Roma alidondoka akiwa na mkuki ule kutoka angani na jambo lile lilimuogpesha zaidi na kwa kutumia kanuni za anga alimshikilia.

Athena mara baada ya kuangalia uso wa Roma ambao umepauka aliweza kugundua Roma alikuwa amezuia andiko la urejesho kutokumponyesha.

Ki ufupi ni kwamba Roma aliacha kila kitu ambacho kinausaidia mwili wake wakati wa majeraha kutofanya kazi , ilikuwa tayari ashaamua kufa, sio kwasababu Athena kamchoma kisu bali ni kwasababu yeye ndio kaamua kufa.

Ilikuwa ni swala la muda tu kupoteza damu yote na mwili wake kuacha kufanya kazi na hatimae kukikaribia kifo.

Ni miujiza tu kwa yeye kuweza kuongea mpaka wakati huo kulinganisha na ukubwa wa jeraha.

Roma ambae alikuwa amezuia uwezo wake wa nishati za mbingu na ardhi hakuwa pia na nia ya

kuifanya nafsi yake kuendelea kuishi , bila msaada wa nishati za mbingu na ardhi nafsi yake taratibu ingetoka katika mwili wake wakati mwili wake na ubongo vitakapo kufa.

Kujiua sio kazi ngumu sana kwa mtu kama Roma ambae alikuwa amepata upeo mkubwa.

Hata kama mtu anamiliki andiko la urejesho , mbinu ambayo ina uwezo hata wa kurudisha maiti kuwa hai , hakuna wa kuweza kumuokoa Roma kama yeye ndio kaamua kufa.

“Ni kweli unataka kufa .. unadhani unastahili kufa kwa ajili yangu?” Athena alionekana kuwa na maneno mengi ya kuongea lakini kuna kitu kilikuwa kimemkaba kooni na kuishia kutingisha kichwa chake

“Haunichukii , Mimi sio Edna wala Seventeen... ni mipango yangu yote ya mimi kukutanisha na Edna na kwanzia wakati huo nilikuwa nikitumia hisia zako kwa Edna na Seventeen kukamilisha

mipango yangu, kwanini umeamua kufanya hivi?” Aliuliza Athena.

“Hata kama wewe sio Edna au Seventeen , bado tu ulimlinda na kumzaa binti yangu ... , haijalishi ulifanya hivyo kwa ajili yangu au lah , ninakushukuru sana , Siwezi kuona nafsi ya mwanamke yoyote ndani yako ikifa , nitaweza vipi kumuua mama wa mtoto wangu kwa mikono yangu miwili , kama nikikuruhusu wewe kuniua vilevile utakosa ujasiri wa kujitokeza mbele ya Lanlan na hilo sitaki litokee , hivyo chaguo sahihi ni mimi kujiua mwenyewe”

Mara baada ya kuhisi uhai wake unazidi kupotea , alijikuta akizidi kutetemeka na nafsi ambazo zilikuwa zimejificha ndani yake zilianza kufurukuta kama kwamba zimekuwa zimefanikiwa kupita katika msukosuko.

Alikuwa katika hali ya mkanganyiko kutokana na hisia zilizokuwa zikiibuka ndani yake , hisia ambazo hakuwahi kuzielewa kabla , ilikuwa ngumu kwake kujidhibiti.

*Huyu mwanaume, inakuwaje hajawahi
kunichukia na bado ananishukuru vilevile?*

Roma alimwangalia kwa macho ya ndani ,
macho yake yalianza kukuosa nguvu na muda
wowote ni kama angepata usingizi.

Kitendo cha mwanamke huyo kulia mbele yake
ni kama kilimpa hali ya kuridhika na kuishia
kutoa tabasamu hafifu.

“Edna...”

Roma aliita kana kwamba alikuwa akimwangalia
Edna akitabasamu mbele yake.

Muda huo kumbukumbu zilizopita zilirudi upya
katika akili yake moja baada ya nyingine kama
vile ni michoro ya kuvutia.

Mwili waAthena ulitikisika, uso wake ulijikunja
kama vile ni mtu anaepitia maumivu, ilionekana
ni kama vile alikuwa akihangaishwa na kitu.

“Ndio , mtu anaempenda ni Edna na Seventeen
na sio mimi kwa hakika, hili halinihusu kabisa ...
kwanini niwe na huzuni kwasababu ya kifo

chake, kwanini nilie kwasababu yake , au ni kwasababu nilikuwa nyuma yake katika maisha yake yote kwa kujificha .. , huu si ndio mwisho ambao nilikuwa niki utumainia , si nimesubiri kwa miaka elfu ishirini kwa ajili ya hii siku .. lakini mbona moyo wangu unauma hivi...”Alikuwa akijiwazia ndani kwa ndani.

Roma hakuwa na uelewa kama nafsi ya Athena ilikuwa ikipitia hali ya mkanganyiko kwa muda huo.

Nafsi tatu zote zilianza kuwasiliana , kuungana, kuamka , kumezana , kugawanyika na kujitofautisha bila kukoma kwasababu ya kuzimwa mwanzoni na kufanya hisia zao kulala.

Ubini wa mwanamke aliekuwa mbele yake haukujalisha kabisa na aliishia kutoa tabasamu tu.

“Edna mke wangu .. uhai wangu umekaribia mwisho , lakini mambo mengi yametokea kati yetu , mengine ni mazuri na mengine ni mabaya

na mengi zaidi siyakumbuki .. lakini nina uhakika wa nyakati nzuri tulizokuwa pamoja ..jambo moja ambalo sijutii na zuri katika maisha yangu , ni kukutana na wewe, Edna hata kama unataka kuniua sasa hivi utabakia kumbukumbu nzuri kwangu , kila kitu kilichotokea leo hii ni maamuzi yangu , ni chaguo langu na haihusiani kabisa na wewe .. usije kuishi maisha ya huzuni na yasio na furaha kwa sababu yangu , kwani itanifanya nijihisi vibaya zaidi nikiwa mfu kuliko nikiwa hai”

Athena kichwa chake kilikuwa kikimuuna sana , kila neno lilikuwa ni kama kisu kinachomkata na kumchoma katika kichwa chake , ilikuwa haiwezekani kujizuia zaidi na aliishia kujilazimisha kuzuia maumivu yake na kulia huku akiuliza;

“Kwanini hukunizuia .. ulijua tokea mwanzo nilichokuwa nikifanya ,, ulijua muda mrefu tu mimi ni nani ,kwanini? , hata kama ni sasa hivi

ungeniambia maamuzi yako , pengine ningeacha , pengine nisingeenda mbali..”

Roma kwa mikono yake yote alishikilia mkuki katika eneo la moyo wake , damu nyingi iliokuwa ikimtoka ilimfanya kupoteza ufahamu na kukosa udhibiti wa mwili wake.

“Kwasababu siwezi”Macho yake yalikuwa nusu yamejifunga huku akicheka kicheko dhaifu.

“Kwasababu siwezi na wewe huwezi , si ulisema mwenyewe hakuna kitakachobadilika mbeleni , umeendeleza misheni yako kwa miaka elfu ishirini , unadhani ni kwa namna gani nitakufanya uache kwa sentensi moja tu , natumia maisha yangu ya miaka ishirini kwa kubadilishana na maisha yako ya miaka elfu ishirini .. hata hivyo haijalishi wewe ni nani , nipo tayari kufanya lolote , hiki ndio kitu pekee ninachoweza kufanya , kitu pekee ninachoweza kufanya kwa ajili yako..”

“No ...!”

Mwanamke huyo alijikuta akishikiria kichwa chake kwa mikono yote miwiili na kukitingisha kwa nguvu, alionekana kukosa mhimili na kuangaua kilio.

Miungu wote walishindwa kujizuia na kuishia kuomboleza kimya kimya wakiangalia tukio hilo.

Roma sauti yake ilikuwa ikidhoofika zaidi na zaidi lakini bado tabasamu halikuwa limetoka usoni.

“Nikishandoka .. naomba usiwasumbue watakao omboleza kifo changu, waambie sina maana tena na wanisamehe .. na zaidi ya yote naomba usimfanye Lanlan kuishi bila mama ... kabla ya kuja hapa nilishamwambia mama yake atarudi..”

“Acha kuongea... Acha kuongea ...!!”

Mwanamke huyo alibembebeza akimtaka Roma asiendeleo kuongea kwani ukichaa ulikuwa ukimvaa , aliishia kujipigia magoti kwenye hewa

mbele yake huku mikono yake ikiwa imemshikilia Roma katika kiuno.

Roma hakuwa na uwezo tena wa kuinua mgongo wake na alijikuta akilegea taratibu , damu ilikuwa imemchafua mwanamke huyo lakini alionekana kutokujali na aliishia kulia kutokana na maumivu.

Hatimae alifumba macho yake na sauti yake haikusikika tena zaidi ya midomo kucheza cheza.

“Edna ... unajua ..unajua , nilishawahi kuwaza mtu pekee anaeweza kuniua itakuwa ni mimi mwenyewe.... siwezi kushindwa na mtu yoyote wala hukunishinda , nimejishinda mimi mwenyewe kwasababu , Edna sikuweza.. sikuweza kukupenda...”

Roma sauti yake haikueleweka alitaka kumalizia kuongea nini lakini huo ndio ulikuwa mwisho wa sentensi isiokamilika , alikuwa ni kama Tiara iliokatika uzi na kupotea kusikojulikana kiasi cha kutokupatikana tena.

Wakati huo mwanamke huyo alijikuta akipumua pumzi ya barafu , alifumbua macho yake na kuinua kichwa chake juu , aliukumbatia vizuri mwili wake ambao tayari ushakuwa wa baridi.

Alimwangalia kwa macho yasio ya kawaida mwili wa mwanaume huyo ambao haukuwa na dalili yoyote ya uhai , alijikuta akiinamisha mdomo wake na kukutanisha na mdomo wa marehemu na kumbusu kwenye lipsi zilizokauka.

Wakati machozi yake ya moto yakiloanisha sura ya mwanaume huyo alijikuta akilazimisha tabasamu.

“Roma mume wangu si nilikuambia kipindi kile , nilikuambia kabisa ukiendelea kubakia na mimi utakufa , nilikuwa nikipata ndoto za kila siku kwa muda mrefu sana lakini bado ukakataa kuamini maneno yangu *Now its too late* , ndoto imekuwa uhalisia lakini bado unaniambia nisiwe mwenye hatia , Hubby kwanini unanifanyia hivi , kwanini unanifanyia matani ya namna hii , unaniogopesha mwenzio , tafadhari

acha kuniogopesha , Amka sasa mume wangu ,
Mimi ni mkeo Edna..”

Kilio cha Edna hakikuwa kikielezeka ni upepo
tu uliofanya asisikike , Aliita majina yote mazuri
kwa ajili ya kumrudisha Roma hai lakini
mwanaume huyo hakuamka kabisa.

* * * * *

Upande wa visiwa vya wafu ndani ya ngome ya
marehemu Hades, Lanlan alionekana akitoka
katika chumba chake huku akichezesha lipsi
zake , alikuwa akipiga miayo na kujinyoosha
nyoosha huku akijiuliza kwanini mashangazi
zake hawajamuamsha siku hio.

Kibonge nyanya huyo alikuwa amepitiliza kulala
muda mrefu siku hio na kumfanya kuhisi njaa
kali.

Lakini hata hivyo alijisiikia vizuri maana
hakukuwa na wa kumlazimisha maswala ya
kusafisha kinywa na kuosha uso wake , isitoshe

alikuwa akichukia usumbufu huo mno , dawa ya meno yenyewe haikuwa tamu.

Akiwa amevalia kijiblauzi cha mikono mifupi na kisuruali cha rangi nyeupe , Lanlan aliangaza kulia na kushoto na kisha kutembea katika vyumba vya mashangazi zake na kila chumba alichopita hakikuwa na mtu.

Hali ya kujikatia tamaa na kutokufurahi ilijionyesha katika uso wake huku akijiambia inamaana kila mtu kaelekea kupata chakula bila kutaarifiwa, lakini mara baada ya kuacha pua zake za utambuzi kunusa hakuweza kupata harufu nzuri ya chakula hata kidogo.

Hatimae fahamu zake zilimwambia aende katika chumba kikubwa, mara baada ya kufika akashika komeo na kuanza kulizungusha lakini mlango ulionekana kufungwa kwa ndani.

Dakika hio hio kwa kutumia uwezo wake wa nishati za mbingu na ardhi aliweza kusikia sauti za pumzi zikisikika kutoka ndani ya chumba

hicho na hazikuwa pumzi ya mtu mmoja bali ya wengi.

“They are all playing hide and seek and ignoring me on purpose!” Aliongea mwenyewe akimaanisha wanacheza mchezo wa kutafutana makusudi tu huku wakimpotezea.

“Puuh!!!”

Nguvu za Lanlan hazikuwa za mchezo mchezo , alijirudisha nyuma kidogo tu na kupiga mlango huo wa chuma kikumbo na loki zake zote zilifyatuka na kuharibika kabisa na kwenda kudondoka kwenye sakafu ya chumba hicho.

“I’m hungry ! Aunties , what are you doing hiding here ?”

Mara baada ya kupiga makelele na kusimama alijua kuna kitu hakipo sawa.

Kitu cha kwanza ni kwamba mashangazi zake wote walikuwa uchi ,walikuwa wamelala bila nguo za kulalia huku kila mtu akilala staili yake katika kitanda hicho kikubwa .

Pili baba yake hakuwepo na kulikuwa na harufu isiokuwa ikielezeka.

Lakini hata hivyo harufu hio haikuwa mpya kwa Lanlan , kwani alishawahi kuinusa wakati baba yake na mama yake wakimaliza kuchukua mazoezi na shangazi zake pia.

Sasa kwasababu bibi yake alimwambia ni jitihada za baba yake kumpatia wadogo zake hakujisumbua sana kufikiria.

Mara baada ya kushika tumbo lake ambalo lilikuwa likinguruma , kama mpira alijirusha na kwenda kutua juu ya kitanda na kuanza kumtingisha mmoja mmoja kwa nguvu.

Hatimae wanawake wote waliamka wakiwa katika bumbuwazi kutokana na ukatili wanaofanyiwa na kashetani hako kadogo , maana hakuwa akichagua sehemu maalumu ya kutingisha.

Mara baada ya wote kuamka na akili zao kukaa sawa walijikuta wakitamani kuingia uvunguni

kutokana na hali waliokuwa nayo , hususani baadhi yao ambao walikuwa na kimiminika kilichogandiana mwilini.

Waliishia kumwambia Lanlan kushuka chini sebuleni akaangalie TV na kisha wakakimbilia kwenye vyumba vyao kwa ajili ya kujisafisha

Kwa wakati huo hakuna ambae alijisumbua kufikiria kile ambacho kinaendelea juu ya Roma na hawakuwa wakikumbuka vizuri lakini walielewa alikuwa amewawekea kitu kilichowafanya kulala muda mrefu.

Wakati wanawake hao wakijishangaa na kujiuliza maswali mengi upande wa Blandina alikuwa akimsaidia Afande Kweka kuzishuka ngazi kuja sebuleni na kisha alianza kuita jina la mwanae Roma.

Ilikuwa tayari ni mchana lakini hakuweza kuona mtu yoyote na hata pale walipojitokeza hakuna ambae alikuwa na ujasiri wa kuongea wapi Roma

alipo licha ya kuwa na hisia juu ya kile
kinachoendelea.

Kila mmoja aliamua kupotezea hali ya wasiwasi
na kujiweka bize kuandaa chakula ili wasimfanye
Lanlan kuzidi kutoa miayo.

Blandina alimjali sana Lanlan kuliko kitu
chochote na alienda jikoni kumchemshia uji
kwanza ili kupunguza njaa.

Crashhh !!!!

Sauti ya bakuli kupasuka ilisikika huku uji wote
ukimwagika chini na vipande kusambaa.

Waliosikia mlio huo walishituka na kukimbia
kuangalia kilichotokea na walishangaa kuona
alikuwa ni mama mkwe wao aliedondosha bakuli
la udongo.

Blandina moyo wake ulikuwa mzito mno ghafla
tu na alilazimisha tabasamu na kuwaambia
kwamba yupo sawa lakini licha ya hivyo mapigo
ya moyo yalikuwa yakienda kasi mno kiasi cha

kukishika kifua chake., kwasababu zisizoeleweka alikuwa akijihisi maumivu.

* * * * *

Upande wa ncha ya kaskazini wingu kubwa jeusi lilikuwa limetanda na upepo ulikuwa mkali mno.

Mti Mama ambao ulikuwa umechukua nafasi kubwa ulikuwa ukipungua ukubwa wake kwa spidi ambayo inaonekana kwa macho.

Matawi na majani yake vilianza kugeuka chembechembe kama za madini ya dhahabu na kupotelea angani , ule ulinzi uliokuwa umezingira mti huo uliweza kupotea pia .

Uuungu ambao ulikuwa katika hatua za ukuaji ulianza kupotea pia kwa kudondoka juu ya mti.

Mti huo mkubwa sana ambao ulikuwa umelitanda anga ulianza kurudi taratibu katika umbo la moyo wa Gaia.

“Its over .. Athena too has lost ..”Christen aliongea huku akiangalia namna Mti mama

ulivyokuwa ukisinyaa akimaanisha imekwisha ,
Athena na yeye ameshindwa.

Miungu muda huo walikuwa wamesimama katika
barafu wakiangalia tukio hilo

“Uungu wa Zeus umepotea , Athena amepoteza
udhibiti wa uungu wake na wa kwetu
umepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na
majeraha , hata kama Mti mama usirudi katika
umbo la moyo wa Gaia hatuna uwezo wa
kuulinda sisi wenyewe , hatuna nguvu
tena” Aliongea Hera akiwa ni mwenye
masikitiko.

Kutokana na ufahamu wao kuungana na Mti
mama , ilikuwa tayari ushahisi kushindwa kwa
miungu ndio maana ukaamua kupotea wenyewe
kwa kurudi katika umbo la Moyo wa Gaia ili
kujificha.

Hio ni mmoja ya njia ya ulinzi binafsi ya mti
mama , pale upatapo misukosuko chaguo la
mwisho la kujilinda ni kurudi katika umbo la

mbegu au moyo na kusubiri nafasi nyingine ya kuota tena.

Muda huo miungu hawakuonekana kuwa ni wenye furaha au huzuni.

Kushindwa ni kushindwa tu , hata kama Roma amepata ushindi huo kupitia kifo chake haikumaanisha kwamba miungu hao walikuwa wameshinda.

Asiwepo hata mmoja , wote waliangalia upande mwingine juu ya barafu kwa mbali.

Edna alikuwa amepiga magoti juu ya barafu , akiwa ameshikiria maiti ya Roma katika mikono yake huku akiwa halii bali mtu aliekuwa amepotelea kwenye mawazo.

Eneo la kifua chake kulikuwa kumebakia shimo kubwa mara baada ya mkuki ule waPalas kutolewa , damu ilishakauka na jeraha kuganda kwa barafu , kuhusu moyo wake ulikuwa ushaharibika na kuwa vipande vpande.

Mwanamke huyo mrembo machozi yalikwisha kumkauka na aliishia kuyaangalia mashavu yaliopauka ya marehemu mume wake bila ya kusema lolote.

Kwa jinsi upepo ulivyokuwa ukipeperusha nywele zake ilimfanya kuonyesha kuwa mpweke sana na kutia huruma na hakuna ambae alimsumbua.

Baada ya muda kidogo hatimae Christen alimsogelea Edna pale alipo na mara baada ya kuangalia sura ya Roma kwa huzuni alimgeukia Edna.

“Wewe ni Edna?”

Edna alikuwa ni kama hajamsikia kwani hakujisumbua hata kujibu swali lake , alichokuwa akifanya ni kumkumbatia Roma kana kwamba hataki mwili wake kugeuka barafu bila kuonyesha hisia zozote.

Hera na wengine wote walifika pia na kuiangalia maiti ya Roma huku wakiwa na hisia zisizoelezeka.

Chuki zao na majonzi yao hayakuwa na tofauti kubwa na kile alichokuwa akijisikia Edna..

Ufufuo wa miungu umeshindikana kiasi cha kuwafanya kuonekana kuchoka pia .

“Aphrodite acha kumsumbua atakuwa anajisikia vibaya sana hapo , naona uungu wa Athena bado upo lakini kwa hiari yake ameamua kuisalimisha nafsi yake kwa Edna”Aliongea Apollo.

“Imewezekanaje? , hata kama Athena hamuwezi Roma lakini haimaanishi hawezi kulinda nafsi yake zidi ya Seventeen na Edna”Aliongea Ares.

“Labda ni kwasababu jina la mwisho alilotamka Roma ni la mke wake Edna”Alijibu Artemis.

“Inaonekana si tu kipindi akiwa katika mwili wa Seventeen au wa Edna , Athena amekuwa na hisia za kimapenzi kwa Roma , inasikitisha

kuona amekuja kulijua hilo sasa hivi na kitu ambacho ameona anaweza kufanya kwa ajili ya Roma ni kuisalimisha nafsi yake kwa Edna”Aliongea Apollo

“Kwahio inamaana sasa hivi Edna ndio mtawala wa uungu wa Athena?!”Aliuliza Hermes akiwa amekunja sura.

“Haha.. una wasiwasi atatuaa sasa hivi , tuna bahati hata hivyo kuwa hai mpaka sasa hivi , kuna haja gani ya kuogopa kifo?”Artemis aliongea kwa kucheka.

Sura ya Hermes ilikakamaa ashindwe kutamka neno.

Lakini muda huo huo hali ya eneo hilo ilibadilika kwa haraka sana.

Anga lilionekana kuchemka na kutengeneza shimo kama ombwe na mwanamke na mwanaume waliweza kuonekana wakitoka , miungu hao hawakuweza hata kuelewa ni kwa namna gani watu hao wamefika hapo.

Watu hao walikuwa ni Aoiline na Sharif.

Mara baada ya Aoiline kuona maiti ya Roma aliishia kutingisha kichwa chake huku muonekano wake ukiwa ni wa kuomboleza , alionekana kuthibitisha ukweli juu ya Roma kupoteza maisha na hakuna uwezekano wowote wa kumponyesha kwasababu kaamua yeye mwenyewe kujiua.

Miungu hao mara baada ya kumwangalia vizuri Sharif , wote walikakamaa huku sura zikijikunja.

“Its you , the one from 20000 years ago!!?”

Miungu kwa haraka sana waliweza kujua mtu huyo ni jini aliehusika kumfungia Zeus katika gereza la roho miaka elfu ishirini iliopita pia mtu ambae alizuia miungu kutokuitawala dunia na kisha kuwasainisha The gods treaty.

Sharif upande wake hakuwa na mudi ya kuwaangalia kabisa na mara baada ya kuiangalia maiti ya Roma aliishia kuonyesha muonekano usioelezeka.

“Mtoto mjinga sana wewe , umeyakatisha maisha yako mwishoni mwa safari , kwanini hutaki kusikiliza maneno ya wakubwa zako?”

Edna hatimae aliinua uso wake kama vile ni mtu alieitambua sauti ya mtu huyo anaongea na hasira zilimvaa palepale.

“Umeridhika na mwisho wa haya matokeo?” Aliongea akiwa hana chembe ya woga hata kidogo.

Mara baada ya Athena kujijisalimisha kwa Edna , ilimaanisha pia kumbukumbu zote za kwake na za Seventeen alizisalimisha pia , hivyo kikawaida Sharif asingekuwa mgeni kwake.

Kama kuna mtu ambae kwa muda huo Edna alikuwa na chuki nae sana basi ni Sharif au Master namba moja , muangalizi wa dunia.

Kama sio kutengeneza mchezo huo wa kimtego , Roma kujitoa kafara kusingetokea.

Edna hata yeye alitamani asingefahamiana na Roma au kipindi kile angeachana nae moja kwa moja.

Lakini hakutaka kujimilikisha nguvu ya Athena ili kupigana na Sharif.

Alijua kabisa kulikuwa na gepu kubwa kati yake na Sharif , hata kama alikuwa akimchukia sana hakuwa na chakumfanya.

Maneno ya Roma kabla ya kifo chake yalikuwa yakigonga katika akili yake , bado alikuwa na mtoto wa kulea na mambo mengi ambayo alihitajika kuyafanya hivyo hakutaka kufa muda huo , alihitaji kuishi kwa ajili ya mambo hayo , kwa ajili ya Lanlan.

“Sikutarajia kama atachukua maamuzi haya ...” Aliongea Sharif huku akionyesha namna gani alikuwa akijutia.

Ijapokuwa miungu wamepoteza pambano juu ya ufufuzi wa miungu wenzao , Roma pia amekufa.

Kwa matokeo hayo ni kama alijikuta akishindwa kufaidika kwa namna yoyote ile , hakumpata mtu wa kuchukua mikoba yake wala miungu kutawala dunia.

Sharif alitamani kama binadamu wangeshinda basi angemrithisha Roma mikoba yake na kuondoka , lakini vilevile kama miungu ingeshinda asingekuwa hata na haja ya kumtafuta mrithi angeondoka kwani alijua uwezo wa kujilinda wao wenyewe wanao, ki ufupi ni kwamba misheni yake imefeli pia.

“Mhmh , kwahio unasema kwamba mimi ndio nilipaswa kufa leo hii na sio mume wangu .. kama ni hivyo basi samahani kwa kukuangusha na tumaini lako kuyeyuka” Aliongea Edna katika hali ya dhihaka.

Sharif upande wake hakutaka kujisumbua na maneno ya dhihaka ya Edna , alichokifanya muda huo ni kuangalia maiti ya Roma kimya kimya akiwa katika hali ya kihisia isioelezeka.

Isitoshe matokeo ambayo aliyasubiria kwa zaidi ya miaka elfu ishirini yalikuwa ni ya kuvunja moyo.

Aoiline hakutaka kumuongelesha Sharif muda huo kwanamna ya kumchokoza , hivyo aliishia kuangalia miungu waliobakia katika hilo eneo kwa sura isiokuwa na utani.

“Mnapaswa kuacha kumkodolea macho huyu mtu , kwa uwezo wenu wa kanuni za anga hata muishi miaka mingine milioni moja hamtomuweza , nawashauri kuishi maisha yenu kwa amani hapa duniani , sehemu ambayo imeathirika na misheni zenu pamoja na mapepo mlioyaachia , kurudi katika hali yake ni jambo litakalochukua muda , kama mnahitaji amani ni kheri mkafanya kitu tofauti na kuendelea kuangalia watu , mmenielewa?”

Miungu hao walijua kabisa mtu ambae anaweza kuongozana na Sharif lazima uwezo wake hautakuwa wa kubezwa hata kidogo , hivyo hawakutaka kutotii maneno yake.

Ilikuwa ni kweli , kama wanataka kuishi hapa duniani vizuri wanapaswa kwenda kuisafisha dunia ambayo wameichafua , iwe wanataka au hawataki , kwa vyovyote vile dunia ni ya binadamu na wao watabakia kuwa wageni.

Mara baada ya kuongea kauli hio Aoiline alimsogelea Edna ambae alikuwa amejichokea na kumshika bega.

“Wewe kuishi vizuri ndio njia nzuri ya kulipia alichokifanya leo hii , naamini hataki kukuona katika hali ya ukiwa” Aliongea.

Edna hakuongea neno zaidi ya kuiinua maiti ya mume wake na kusimama.

Alimwangalia Sharif kwa macho makali mno kama kwamba alikuwa akimwambia inaweza isiwe leo ila siku nitakuua na kisha aligeuka na kuianza safari.

Alikuwa na mpango wa kumrudisha Roma visiwa vya wafu ili kuzikwa na aishi hapo hapo ili alione kaburi lake kila siku.

Mjane huyo alisababisha hali kuwa ya huzuni na ukimya usio wa kawaida , kwa namna alivyoupakata mwili wa Roma ilisikitisha sana kwa wale waliokuwa wakimwangalia.

ITAENDELEA SAA NANE.